# MAONI & UCHAMBUZI

## Nukuu



Nakubali kushindwa, kila mmoja hushindwa katika jambo fulani. Muhimu ni kujaribu tena na tena.

**Michael Jordan, mchezaji wa mpira wa kikapu Marekani.**

## Viongozi wa dini wamenena, kukosoa si upinzani

Juzi viongozi wa dini nchini walitoa ya moyoni wakitaka wasionekane wapinzani pale wanapokosoa mabaya ya Serikali. Wala wasionekane wametumwa na chama chochote cha upinzani kutoa msimamo wao binafsi kwani wanachokifanya sehemu ya huduma yao.

Tunaungana na viongozi hawa wa dini kutaka dhana hii potofu ipingwe na isitumike kuligawa Taifa ambalo Katiba yake ya mwaka 1977 inatoa uhuru wa mtu yeyote kueleza anachokiamini bila kuvunja sheria.

Kwenye mkutano wa viongozi hao wa dini uliofanyika jijini Dar es Salaam, .wametaka waeleweke zaidi kwa watu kutafakari wanachokisema badala ya kuchukuliwa ni wapinzani kila wanaposema ukweli au kutoa mtizamo tofauti na mtizamo wa wengine.

Viongozi wa dini, kama walivyo wanasiasa, wafanyabiashara na wawekezaji, wasanii na wanamichezo, ni kundi muhimu katika ujenzi wa Taifa imara na walikutana hapo kujadili nafasi yao katika kudumisha amani na maendeleo baada ya uchaguzi mkuu wa Oktoba 28.

Viongozi hawa wanaamnini kukaa kimya sio suluhisho kwa machungu yanayoendelea kwenye jamii bali kuzungumza kutaleta ufumbuzi na amani ya kudumu.

Kila mmoja anafahamu yaliyotokea kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka huu ambao CCM kimeibuka na ushindi mkubwa wa kihistoria lakini unaolalamikiwa na wapinzani wake.

Baadhi ya vyama vimejaribu kuomba msaada wa kimataifa na vingine kuwazuia wabunge wake wa viti maalumu kuapa ili kuwakilisha masilahi ya chama husika. Viongozi hawa wanaamini kukaa kimya hakutoleta tiba ya makovu yaliyopo kwa wananchi. Wanaona ipo haja ya kuzungumza na kila mmoja atoe mtizamo wake.

Wao wanaamini maendeleo hayawezi kupatikana kukiwa na watu wanaonung'unika ilhali wanatakiwa kushiriki katika kuyajenga maendeleo hayo. Uchaguzi mkuu umemalizika -lakini wengi hawana furaha.

Huu ni ukweli unaoonekana kwa mtu yeyote asiyefikiri kwa itikadi ya chama cha siasa hivyo watakaokuja kupinga ni wenye mrengo na chama fulani hata kama haamini anachokisema.

Tumefika mahali ambapo baadhi ya viongozi wa kisiasa kila anayekosoa mapungufu yaliyopo serikalini basi si mzalendo. Kwao mzalendo ni anayesifia na kupongeza.

Kama walivyosema viongozi hawa, uchaguzi umemalizika lakini wapo watu wana manung'nuko...ndani ya chama tawala hata upinzani. Tunaunga mkono kwamba kuacha watu waongee kutasaidia kutibu makovu ya uchaguzi mkuu.

Ndio maana hata Waziri Mkuu mstaafu, Jaji Joseph Warioba ametaja kasoro nne za uchaguzi mkuu huo na akashauri zishughulikiwe ili kuliwezesha Taifa kuendelea kuwa na amani.

Moja ya kasoro hizo ni suala la Tume kuengua wagombea na mawakala, suala la mwanachama kukubalika ili ateuliwa na chama halizingatiwi, haki za binadamu kuvunjwa na vurugu katika uchaguzi wa Zanzibar.

Wote, Jaji Warioba na viongozi wa dini si wapinzani bali wanatumia haki yao ya kikatiba kutoa maoni na mitizamo yao jambo linalopaswa kuhamasishwa nchini katika safari yetu ya kujenga uchumi imara.

## KIPANYA




**HUTOLEWA NA MWANANCHI COMMUNICATIONS LTD**

Barabara ya Mandela, SLP 19754, Dar es Salaam.
+255 22 24 50875, 0754 780647
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

**Bakari Machumu:** Kaimu Mkurugenzi Mtendaji/ Mhariri Mtendaji Mkuu
**Angetile Oslah:** Mhariri Mtendaji




MUSSA JUMA

## Kuwe na usawa katika kumiliki ardhi

Mfumo dume na baadhi ya mila na utamaduni uliopitwa na wakati ni kikwazo kwa wanawake hasa wa vijijini kumiliki ardhi.

Ingawa wao ndio watumiaji wakubwa wa ardhi kwa shughuli za kilimo, wengi hawana haki ya kuimiliki. Ni ngumu kwa wanawake kumiliki ardhi vijijini hata wachache wanaobahatika, huipatia mahakamani.

Kuna sababu nyingi zinazochangia hali hii ukiwamo mfumo dume, mila na desturi pamoja na wanawake wengi kutopewa elimu ya kutosha.

Licha ya jitihada zinazofanywa na Serikali na asasi za kiraia kutoa elimu juu ya umiliki wa ardhi bado tatizo ni kubwa nchini.

Jamii zilizoathirika sana na tatizo hili ni za kifugaji ambako kwao kusikia wanawake wanaweza kumiliki ardhi ni sentensi ngumu kuielewa.

Ingawa jamii ya sasa imeathiriwa sana na mabadiliko ya tabianchi yaliyosababisha kupungua kwa idadi ya mifugo kutokana na kukosa malísho hivyo jukumu la ulezi wa familia kubaki kwa wanawake, bado changamoto ni kubwa.

Utafiti uliofanyika katika wilaya za Ngorongoro, Monduli na Longido mkoani Arusha, umebaini iwapo hatua hazitochukuliwa mapema, haki ya kumiliki ardhi kwa wanawake itaendelea kuwa ndoto.

Hata wanawake wachache waliopo wanaotambua haki yao ya kumiliki ardhi wanaendelea kunyanyasika licha ya kushinda kesi zao katika mabaraza ya ardhi na mahakamani.

Wilayani Ngorongoro, baadhi ya wanawake wamepambana na kushinda kesi za kumiliki ardhi lakini wameishia kutengwa.

Wanawake hawa wanatengwa kwa kuonekana wanafanya mambo ya aibu kupambana na wanaume.

Baadhi ya wanaume kwa kutumia nafasi zao katika jamii wamekuwa kikwazo cha kuwapa haki hii ya kiuchumi wanawake.

Hata hivyo, Serikali na wadau wanabainisha haja ya kukaa pamoja na kubadili mtizamo huu hasi dhidi ya wanawake.

Mjadala wa haki ya kumiliki ardhi kwa wanawake unaweza kuanzia katika familia, mikutano ya kijiji ikaendelea mpaka ngazi ya wilaya na mkoa.

Katika mijadala hii ni muhimu usawa ukajadiliwa sambamba na faida zinazoweza kupatikana kama wanawake wakisimamia ardhi walizorithishwa au kuachiwa na wenza wao.

Ni ukweli uliowazi kuwa mchango wa wanawake katika jamii ni mkubwa hasa kutokana na uwezo wao mkubwa kulinda na kusimamia mali za familia.

Wanawake ni walezi wazuri wa familia, ndio walinzi wa mali za famila kutokana na kuwa nyumbani na watoto kwa muda mwingi zaidi tofauti na wanaume.

Katika jamii za wafugaji zinazokabiliwa na uhaba wa ardhi, wanawake hawaruhusiwi kuuza ardhi waliyonayo kwa maelezo ya kulinda haki ya watoto na mifugo.

Ni muhimu sheria na sera zetu zikaendelea kuboreshwa ili kuweka usawa wa umiliki wa ardhi katika jamii.

Sheria zetu zikiondoa upendeleo wa umiliki ardhi basi wanawake watapata haki sawa na wanaume na kuwa na sauti katika ardhi ya familia.

Ingawa kuuza ardhi ya familia kuna utaratibu wake unaohakikisha wanawake wanashirikishwa kwa kutoa ridhaa kwa familia lakini bado jambo hili limekuwa gumu kutekelezwa na familia nyingi.

> **Wakulima wadogo ambao wengi ni wanawake, ndio wanaoilisha Tanzania hata kuzalisha chakula cha ziada kinachouzwa nje ya nchi au kutolewa msaada kwa wahitaji.**

Itoshe kwa kutoa wito wa kuwapo mijadala kuanzia katika kaya juu ya haki ya umiliki ardhi lakini pia jambo hili litawezekana kama wanaume watakubali kuanza kuandika wosia wa mgao wa mali zao ikiwapo ardhi kwa kuwamilikisha watoto wao wa kike.

Ni muhimu pia Serikali na asasi za kiraia kuongeza nguvu katika kuwajengea uwezo wanawake kujua haki yao ya kumiliki ardhi.

Kwa kuwa bado kuna mila na tamaduni kandamizi dhidi ya wanawake, unahitajika mjadala wa kudumu katika vikao vya vijiji mpaka Taifa ili kutoa haki sawa ya umiliki mali katika jamii.

Kuimarisha uchumi wa Tanzania iliyoingia kwenye orodha ya mataifa yenye uchumi wa kati tangu Julai mosi mwaka huu kunahitaji ushiriki wa watu wote wakiwamo wanawake wa vijijini. Na kama takwimu zinavyoonyesha, Watanzania wengi wanategemea kilimo na wanawake ndio vinara katika sekta hivyo hivyo wasitengwe.

***Mussa ni mwandishi mwandamizi wa gazeti hili mkoani Arusha. Kwa maoni na ushauri anapatikana kwa 0754 296 503.***